

# Maswali ya Usalama wa Bidhaa kwa Makampuni Yanayojishughulisha na Mbolea za Aina ya Naitrojeni

## Usalama katika Maeneo ya Uzalishaji:

- ① Je, mratibu wa usalama kwenye maeneo ya uzalishaji ameteuliwa?
- ② Je, kuna mpango wowote wa usalama kwenye maeneo ya uzalishaji?
- ③ Je, mpango huo wa usalama una masharti yoyote (ya kisheria) kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki za kiusalama?
- ④ Je, kuna udhibiti wowote wa upatikanaji wa bidhaa hizo kwa watu na vyombo vya usafiri?
- ⑤ Je, upatikanaji wake ni kwa watu waliruhusiwa tu?
- ⑥ Je, kuna utunzaji wa kumbukumbu za mali ghafi, zilizochakatwa na bidhaa zilizohifadhiwa?
- ⑦ Je, kuna mfumo wowote unaotumika kutoa taarifa na kutunza kumbukumbu kuhusu viashiria vyovyote vya kutiliwa shaka na wizi?



## Usalama katika Usambazaji:

- ① Je, mratibu wa usalama kwa ajili ya usambazaji ameteuliwa?
- ② Je, kuna mpango wowote wa usalama katika usafirishaji, usambazaji, na uhifadhi wa nje?
- ③ Je, mpango huo wa usalama una masharti yoyote kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki za kiusalama?
- ④ Je, ni watu walioruhusiwa pekee ndio wanaoweza kuzifikia hifadhi za nje na wasambazaji?
- ⑤ Je, kuna utunzaji wa kumbukumbu za bidhaa kwenye hifadhi za nje na wasambazaji?
- ⑥ Je, uchukuaji wa bidhaa kutoka kwenye maeneo ya uzalishaji na hifadhi za nje unafanywa na wateja wanaotambulika na watoa huduma wenye sifa za kipekee na nyaraka zinazohitajika, na je, watu hao wana vibali vinavyohitajika?
- ⑦ Je, kuna uthibitisho/uhakiki (na utunzaji kumbukumbu panapohitajika) wa vitambulisho vya wasafirishaji/madereva kwenye maeneo ya uzalishaji/ya kupakia mizigo?
- ⑧ Je, kuna udhibiti wowote wa namna ya kuzifikia meli na mashua zinapokuwa bandarini?
- ⑨ Je, kuna mfumo wowote unaotumika kutoa taarifa na kutunza kumbukumbu kuhusu viashiria vyovyote vya kutiliwa shaka na wizi?

## Usalama katika Mauzo:

- ① Je, ni wasambazaji/watumiaji waliobainishwa/wanaotambulika pekee ndio wanaouziwa bidhaa?
- ② Je, mauzo kwa njia ya mtandao hufanywa kwa wateja waliothibitishwa na wenye akaunti?
- ③ Je, mnatunza kumbukumbu za mauzo yaliyofanywa na bidhaa zilizotolewa kupelekwa kwa wateja?
- ④ Je, kuna mfumo wa kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa za miamala yenye kutiliwa shaka?
- ⑤ Je, mna mfumo wa usalama na taratibu za kupeana taarifa za kiusalama na wafanyakazi wako, na wateja?

